Understanding Immigration Bonds - Swahili

**Je, dhamana ya Uhamiaji ni nini?**
Dhamana ni fedha zinazotolewa kwa Idara ya Usalama wa Taifa ili kuwahakikishia kwamba ukiachiliwa, utarudi kortini kwa vikao vya mahakama vijavyo (na mikutano na ICE).

**Dhamana ni ngapi?**
Kulingana na sheria, dhamana ya chini kabisa inayowezekana kuitishwa ni $1,500. Hakuna kikomo cha juu. Katika Minnesota, dhamana za kawaida huwa katikati ya $5,000-$15,000, lakini bado zinaweza kuzidi kiasi hicho.

**Nitaombaje dhamana?**
- Unaweza ulizia dhamana kutoka kwa ICE. Wakikuambia bei ya dhamana, utailipa halafu utaachiliwa. Wakikataa kukupa dhamana ama huwezi kumudu bei wamekuwekea, unaweza kuulizia kikao cha dhamana mbele ya hakimu wa uhamiaji. Kuulizia dhamana mbele ya hakimu haimaniishi kwamba utapewa dhamana. Ni lazima uthibitishe kesi lako.
- Pia, unaweza kuuliza hakimu wa uhamiaji kama anaweza kupunguza bei ya dhamana iliyowekwa na ICE. Lakini, kumbuka ya kwamba hakimu anaweza punguza dhamana, iache jinsi ilivyo, ipandishe, ama aamue ufungwe bila dhamana.

**Je, nahitaji mwanasheria (wakili) wa kunisaidia?**
- Una haki ya kuzungumza na wakili, lakini sio lazima uwe na wakili. Mahakama haitakupea wakili. Kama unahitaji wakili, lazima ujitafutie. Hakimu anaweza kukupa orodha ya mawakili wanaoweza kukusaidia bila kulipwa, lakini itabidi uwasiliane nao wewe mwenyewe ili kuona kama watachukua kesi yako. Sio lazima wachukue kesi yako. Hufai kulipa pesa ili kupigia mashirika hayo simu kutoka kwa jela.

Pia kuna mawakili wa kibinafsi ambao hawako kwa orodha ya mahakama na wanaweza kuchukua kesi za dhamana.

- Kwa kawaida, watu hufaulu zaidi katika kesi zao za dhamana au za kufukuzwa nchini kama wakona wakili. Itasaidia sana kuongea na wakili kabla uamue kama utamwajiri ama utajisimamia. Sio lazima uajiri ama uzungumze na wakili
- Ikiwa huna uhakika kama unahitaji wakili, ama bado hujaweza kumwajiri, unaweza kuulizia muda zaidi kutoka kwa hakimu. Hakimu atakupa muda zaidi wa kuzungumza na wakili. Ukiulizia muda zaidi, hakimu anaweza kukuambia kwamba utengeneze ombi jipya la dhamana ukiwa tayari. Kesi yako ya uhamiaji itaendelea kuzungumziwa kwa muda ambao umefungwa na unatafuta wakili - mahakimu hawatakupa muda usio na kikomo.

**Hakimu ataamuaje kuhusu dhamana yangu?**
Hakimu ataangalia vigezo vitatu kabla aamue kama utapewa dhamana:
- <u>Kwanza, ataangalia kama unastahiki ya kupewa dhamana</u>. Baadhi ya hukumu za uhalifu kama uhalifu wa dawa za kulevya na uhalifu uliokithiri, zinaweza kukunyima fursa ya kupewa dhamana. Huwezi pewa dhamana ikiwa ulifungwa wakati ambao ulikuwa unaingia Marekani, ikiwa umewahi kufukuzwa nchini, ama ikiwa ukona agizo la mwisho la kufukuzwa nchini.

- <u>Ya pili, ataangalia kama wewe si hatari kwa umma.</u> Hakimu atatoa uamuzi kulingana na historia lako la uhalifu. Ataangalia kama uko na hukumu za uhalifu, kama umewahi kufungwa, kama uko na kesi za uhalifu ambazo hazijakamilishwa, ripoti za polisi, ama ushahidi unaoonyesha kwamba umejirekebisha au ushahidi wowote unaotolewa. Ikiwa hakimu anadhani utahatarisha wengine, hutapata dhamana.
- <u>Ya tatu, atahakikisha kwamba hutatoroka</u>. Hakimu ataangalia kama uko na uhusiano na jumuia yako, kama unastahiki kupewa unafuu, na kama umehudhuria kesi zako zingine mahakamani. Hayo yote yatawahakikishia kwamba utahudhuria vikao vyako vyote vya kufukuzwa nchini siku za usoni hata kama umeachwa kutoka kizuizini.

**Je, nitawezaje kumshawishi hakimu anipe dhamana ?**

- Hakimu atakuambia kwamba ukona “mzigo wa uthibitisho” (“burden of proof”). Hii inamaanisha unafaa kuonyesha hakimu kwamba hauhatarishi wengine na hutatoroka. Serikali inaweza kuwasilisha ushahidi wowote unaoonyesha mbona wanaamini unapaswa kubaki kizuizini.
- Hakimu atataka ushahidi kwa maandishi, kutoa neno lako pekee haitoshi. Ushahidi muhimu utakaosaidia sana ni vyeti vya kuzaliwa ama kadi za kijani (green card) za ukoo wako, hati za malipo, mkataba wa kukodisha nyumba uliotiwa saini ama barua inayoonyesha mahali unaishi, barua za kukuungia mkono kutoka kwa ukoo wako, makasisi, waajiri, marafiki, na uthibitisho unaoonyesha kwamba umejirekebisha. (Unaweza kuulizia kijitabu kinachokuelezea jinsi ya kuwasilisha ushahidi unaofaa.)
- Nyaraka zote zinazopewa kwa mahakama kwa ajili ya kesi yako lazima zinadikwe katika Kiingereza au ziunganishwe na tafsiri iliyothibitishwa.
- Ni ngumu kukusanya ushahidi wakati ambao uko kizuizini. Familia yako ama wakili wanaweza kukusaidia. Wakili anaweza kukusaidia kukagua habari na uthibitisho zitakazofaa zaidi katika kesi yako. Pia, wakili atakusaidia kutafsiri nyaraka zako za dhamana.

**Hakimu akinipa dhamana amabayo siwezi kumudu, nifanye nini?**

- Sio lazima ulipe dhamana wakati huo huo. Pia, sio lazima ulipe dhamana wewe mwenyewe - mtu yeyote aliye na uthibitisho halali wa Marekani anaweza kukulipia dhamana. Lakini, hutaachiliwa mpaka dhamana ilipwe.
    - Kumbuka, ikiwa mtu anakutisha ama anatisha wapendwa wako ndiyo akupe pesa za dhamana, unafaa kuwasiliana na wakili wa uhamiaji kuiripoti. - Sheria hairuhusu mtu yeyote kukulazimisha ama kulazimisha wengine wafanye kazi au vitendo vya ngono ili walipe dhamana yako.
- Hazina ya jumuiya inayoitwa, The Minnesota Freedom Fund, labda itaweza kukulipia dhamana. Mtu atahitaji kuiulizia kwa niaba yako, kwa kwenda katika tovuti ifuatayo: mnfreedomfund.org

**Hakimu akikataa kunipea dhamana, nini itafanyika?**

- Utapewa kikao kimoja tu cha dhamana. Usipopewa dhamana, utabaki kizuizini hadi kesi yako ya kufukuzwa nchini ikamilike. Isipokuwa kuwa mabadiliko makubwa katika hali yako, kama vile kufutwa kwa mashtaka yako ya uhalifu ama hukumu kufutwa, hutapata

kikao kingine cha dhamana hakimu akikataa kukupa dhamana. Hii ndiyo maana unafaa kujitayarisha kwa kikao chako kimoja cha dhamana.
- Unaweza kukata rufaa kwa uamuzi wa hakimu. Hii inamaanisha kwamba unafaa kuuliza mahakama ya juu zaidi, kama Bodi ya Rufaa ya Uhamiaji ( Board of Immigration Appeals, BIA), ndiyo wakague kesi yako. BIA inaweza kubadilisha au kukubaliana na uamuzi wa hakimu. Ukitaka kukata rufaa, hakimu atakupa karatasi unazohitaji kujaza na maelekezo zaidi. Utabaki kizuizini kwa muda ambao rufaa itakapozungumziwa.

**Je, pesa yangu ya dhamana itarudishwa?**
- Ukihudhuria vikao vyako vyote mahakamani na ufuate maagizo yote yanayowekwa na Hakimu wa Uhamiaji ama ICE, tena uondoke nchini ukiagizwa, pesa ya dhamana itarudishwa kwa mtu ambaye alilipa kesi ikikamilishwa. Lakini ICE wanaweza kukataa kurudisha dhamana ikiwa hukuenda mahakamani ama hukufuata maagizo uliyopewa.

**Kumbuka**
- Mahakamani, kikao cha dhamana ni tofauti na kikao cha kufukuzwa nchini. Kama unataka mkutano wa dhamana, lazima uuulizie. Unaweza kuuliza kwa maandishi ama kwa kuuliza hakimu unapoenda mahakamani.
- Utapewa kikao kimoja tu cha dhamana, kwa hivyo uwe umejitayarisha na ushahidi.
- Sio kila mtu atapewa dhamana. Sheria ya uhamiaji inasema baadhi ya watu hawafai kupewa dhamana. Pia hakimu wa uhamiaji anaweza kuamua kwamba hufai kuachiliwa na atakataa kukupa dhamana.
- Haijalishi kama ombi lako la dhamana limekataliwa ama limekubaliwa, kesi yako ya kufukuzwa nchini itaendelea kama umefungwa au umeachiliwa kwa dhamana.
- Kesi yako ya uhamiaji ni tofauti na kesi zako zozote zingine za wakati huu, zijazo, ama zilizopita. Ni mahakama tofauti, iliyo na mahakimu tofauti na mawakili tofauti. Ukipata dhamana katika mahakama ya uhalifu, haimaanishi kwamba utapata dhamana katika mahakama ya uhamiaji. Pesa yoyote itakayolipwa kwa dhamana ya uhalifu, haitaenda kwa dhamana yako ya uhamiaji.
- Sio lazima uwe na wakili, lakini watu hufaulu zaidi katika kesi zao kama wakona wakili.

Hati hii iliundwa na The Advocates for Human Rights, Minneapolis, MN. Sio mbadala wa ushauri wa kisheria. © Desemba 2021